Nambari ya Mtahiniwa _____

SMZ

BARAZA LA MITIHANI LA ZANZIBAR

MTIHANI WA KUINGILIA KIDATO CHA TATU

021 KISWAHILI

MUDA: SAA 2.30 JUMATANO 23 DISEMBA, 2020 MCHANA

MAAGIZO KWA WATAHINIWA

1. **Mtihani huu una sehemu NNE (4) A, B, C, na D.**
2. **Jibu maswali YOTE kutoka sehemu A, maswali MAWILI (2) kutoka sehemu B, maswali MAWILI (2) kutoka sehemu C na swali MOJA (1) kutoka sehemu D.**
3. **Andika nambari yako ya mtihani katika kila ukurasa.**
4. **Majibu yote yaandikwe kwenye sehemu zilizoachwa wazi.**
5. **Majibu yote yaandikwe kwa kalamu ya buluu au nyeusi.**
6. **Simu za mkononi na vitu visivyoruhusiwa havitakiwi ndani ya chumba cha mtihani.**

KWA MATUMIZI YA WASAHIHISHAJI		
NAMBARI YA SWALI	**ALAMA**	**SAINI**
1.		
2.		
3.		
4.		
5.		
6.		
7.		
8.		
9.		
10.		
JUMLA		

Mtihani huu una kurasa 14 zenye maandishi

Nambari ya Mtahiniwa _____

SEHEMU A: (Alama 20)

UFAHAMU

Jibu maswali YOTE katika sehemu hii.

1. Soma kwa makini beti za shairi lifuatalo, kisha jibu maswali yanayofuata chini yake.

Si leo toka zamani, mkulima mtu **duni**,
Ana tabu maishani, tena hapewi thamani,
Yafaa tutizameni, kisha tuyachunguzeni,
Si leo toka zamani, mkulima mtu duni.

Jogoo linapowika, kokoriko mitaani,
Mkulima huamka, jembe lake mkononi,
Bila ya kupumzika, hufika kwake shambani,
Si leo toka zamani, mkulima mtu duni.

Tena mvua na jua, humwangukia mwilini,
Mkulima huugua, kwa kazi kuithamini,
Mimea **kupalilia**, kukwepa umasikini,
Si leo toka zamani, mkulima mtu duni.

Wakaazi wa mjini, na wafanyakazi pia,
Na viongozi nchini, huduma awapatia,
Sijui kakosa nini? thamani kutomtia,
Si leo toka zamani, mkulima mtu duni.

Maisha ya mkulima, humalizika tabuni,
Haonji malazi mema, kila siku vibandani,
Wenye baba na yatima, wote wako mashakani,
Si leo toka zamani, mkulima mtu duni.

Starehe kwa ujumla, zinaishia mijini,
Maji safi ya muala, njia na umeme ndani,
Aliyezichuma **hela**, ni mkulima shambani,
Si leo toka zamani, mkulima mtu duni.

Dharau wakielewa, kuna hatari mbeleni,
Mkulima **ang'amua**, naye akae mjini,
Hapo ndipo tutajua, mkulima naye nani,
Si leo toka zamani, mkulima mtu duni.

Nambari ya Mtahiniwa _____

MASWALI

a) Ni jambo gani kubwa linalozungumzwa katika shairi hili?

_____

_____

b) Eleza jitihada mbili (2) anazochukua mkulima ili kupambana na umasikini.

_____

_____

_____

_____

c) Bainisha tofauti iliyopo kati ya maisha ya mjini na vijijini.

_____

_____

_____

d) Onesha athari inayoweza kujitokeza endapo jamii haitomthamini mkulima.

_____

_____

_____

_____

e) Eleza maana ya maneno yaliyopigiwa mstari kama yalivyotumika kwenye shairi ulilolisoma hapo juu.

_____

_____

_____

_____

_____

_____

2. Fupisha shairi ulilolisoma hapo juu kwa aya moja (1) yenye maneno yasiyozidi ishirini (20).

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

SEHEMU B: (Alama 30)

SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA

Jibu maswali MAWILI (2) katika sehemu hii. Swali la TANO (5) ni la lazima.

3. a) Toa mfano mmoja (1) kwa kila kielezi cha namna kifuatacho.

   i) Kielezi cha namna kikariri.

   _____

   ii) Kielezi cha namna kiigizi.

   _____

   b) Tumia maneno yafuatayo yasimame kama vivumishi katika sentensi.

   i) Wangu

   _____

   ii) Wale

   _____

   c) Ainisha maneno yanayounda tungo zifuatazo.

   i) Kaka Ali anacheza bao.

   ii) Hapa si pazuri.

d) Geuza sentensi zifuatazo katika kauli ya kutendana.

i) Mzee alimpiga mwanawe.

_____

ii) Askari alimshika mwizi barabarani.

_____

e) Fafanua kwa kutumia mifano aina zifuatazo za unominishaji.

i) Nomino kutokana na kivumishi.

_____

_____

_____

ii) Nomino kutokana na kitenzi.

_____

_____

_____

4. a) Nyumbua maneno yafuatayo na kuunda maneno manne (4) kwa kila neno.

i) Omba

_____

_____

ii) Zima

_____

_____

b) Andika visawe vya maneno yafuatayo.

i) malengo

_____

ii) kuwasili

_____

c) Tofautisha kwa kutumia mifano dhana ya shina na mzizi katika neno.

_____

_____

_____

_____

_____

d) Eleza faida mbili (2) za kuongeza istilahi na msamiati katika lugha ya Kiswahili.

_____

_____

_____

_____

e) Andika dhima mbili (2) za kiambishi awali **''a''** katika neno ''anapendeza".

_____

_____

5. a) Bainisha mambo makuu mawili (2) yanayosababisha mitindo mbalimbali ya lugha.

_____

_____

_____

b) Taja hasara mbili (2) za misimu katika lugha.

_____

_____

_____

c) i) Nini maana ya mawasiliano?

_____

_____

_____

ii) Eleza dhima mbili (2) za lugha katika mawasiliano.

_____

_____

_____

_____

d) Onesha mambo mawili (2) yanayosababisha utata katika lugha ya Kiswahili.

_____

_____

_____

_____

e) Andika kifupisho kinachotumika katika Kamusi ya Kiswahili Sanifu kwa kila neno kati ya maneno yafuatayo. Nambari moja (i) imetumika kama mfano.

NENO	i) kwa mfano	ii) kidini	iii) aghalabu	iv) Fizikia	v) kama vile
KIFUPISHO	k.m				

SEHEMU C: (Alama 30)

FASIHI

Jibu maswali MAWILI (2) katika sehemu hii. Swali la SITA (6) ni la lazima.

6. Tunga igizo fupi linalohusu mapambano dhidi ya udhalilishaji wa watoto.

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

7. a) Tegua vitendawili vifuatavyo.

   i) Nina ng'ombe wangu nisipomshika mkia hali majani.

   _____

   ii) Kisima kidogo kimejaa changarawe.

   _____

   b) Bainisha vipengele vya fani vilivyotumika kuunda methali zifuatazo.

   i) Siri ya mtungi aijuaye kata.

   _____

   _____

   _____

   ii) Bandu bandu humaliza gogo.

   _____

   _____

   _____

   c) Andika mambo mawili (2) muhimu yanayohitajika wakati wa uwasilishaji wa fasihi simulizi.

   _____

   _____

   _____

   d) Taja nyenzo moja (1) muhimu inayotumiwa na msanii kwa kila tanzu ya sanaa ifuatayo.

   i) Ufinyanzi

   _____

   ii) Fasihi

   _____

   e) Fafanua kwa mifano tamathali za semi zifuatazo.

   i) Sitiari

   _____

   _____

   _____

ii) Tashihisi

_____

_____

_____

8. a) Eleza jinsi gani fani na maudhui hutegemeana katika kazi ya fasihi.

_____

_____

_____

_____

_____

_____

b) ”Uhifadhi wa kazi za fasihi simulizi kwa njia ya kompyuta unaweza kuleta matokeo hasi na chanya”. Thibitisha kwa kutumia hoja mbili (2) kwa kila upande.

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

c) Onesha sababu mbili (2) za kuhakiki kazi za fasihi.

_____

_____

_____

_____

_____

d) Eleza kanuni zifuatazo za utunzi wa mashairi ya kimapokeo.

i) Muwala

_____

_____

_____

ii) Utoshelevu

_____

_____

_____

e) Taja sifa mbili (2) za ngano.

_____

_____

_____

_____

SEHEMU D: (Alama 20)

UANDISHI

Jibu swali MOJA (1) tu katika sehemu hii.

9. Eleza mambo matano (5) ambayo mwandishi wa Insha anatakiwa kuyazingatia ili kuifanya Insha yake kuwa bora.

AU

Andika Insha ya maneno 120 hadi 150 ukitetea hoja inayosema "Kuelimika kwa mwanamke ni kuelimika kwa jamii nzima".

_____

_____

_____

_____

10. Andika barua kwa rafiki yako aliyekuweko Singida na umuarifu kuhusu mipango yako ya maisha baada ya kumaliza masomo. Jina lako ni Abebwaye Hujikaza.

Nambari ya Mtahiniwa _____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

.....